# Wizara ya Kazi ya Marekani

# Matokeo ya Mwaka 2018 juu ya Aina Mbaya zaidi za Ajira kwa Watoto

## Tanzania

Mnamo mwaka 2018, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipiga hatua ndogo katika juhudi za kuondoa aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto. Serikali ilifanya juhudi kwa kuanzisha Sera mpya ya Kitaifa ya Ajira kwa Watoto na kuendelea kuunga mkono Mpango wa Mfuko wa Fedha wa Uhamasishaji wa Jamii kuhusu Uhamishaji wa Fedha Taslimu ulio na Masharti nchini Tanzania, huku ikipanga Awamu ya IV kuzinduliwa mnamo mwaka 2019. Hata hivyo, licha ya hatua hizo za kushughulikia ajira kwa watoto, Tanzania iliendelea kufuata utaratibu ambao unacheleweshа kusonga mbele kwa utokomezaji wa aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto. Serikali ya Bara inaunga mkono waziwazi ufukuzaji wa mara kwa mara wa wanafunzi wanaopata mimba kutoka shule za umma, huku ikiwafanya wakumbwe kirahisi na aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto. Watoto nchini Tanzania hushiriki katika aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa madini, uchimbaji wa mawe na kazi za majumbani. Watoto pia hufanya kazi hatarishi katika kilimo. Mapungufu mengine yamebaki katika mfumo wa kisheria na utekelezaji wa sheria zinazohusiana na ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na kinga kwa ushiriki wa watoto katika shughuli haramu na kazi za majumbani; ukosefu wa idhini kwa wakaguzi wa kazi kukadiria adhabu; na uwezekano wa kuwepo idadi pungufu ya wakaguzi wa kazi ikilinganishwa na ukubwa wa nguvukazi ya Tanzania.

Kwa kuzingatia na ripoti hiyo, hatua zilizopendekezwa zimetambuliwa kuwa zingeweza kusukuma mbele juhudi za ukomeshaji wa ajira kwa watoto nchini Tanzania.

| Eneo | Chombo Husika | Hatua Iliyopendekezwa | Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa |
|---|---|---|---|
| Mfumo wa Kisheria | | Hakikisha kwamba vigezo vya ulinzi wa kiwango cha chini cha umri vinatumiwa kwa watoto wanaofanya kazi za majumbani. | 2013 – 2018 |
| | Tanzania Bara | Haramisha utumiaji wa watoto katika shughuli haramu, hasa katika kutengeneza na kuuza madawa ya kulevya. | 2012 – 2018 |
| | | Haramisha uandikishaji wa watoto chini ya umri wa miaka 18 unaofanywa na vikundi vyenye silaha visivyo vya serikali. | 2016 – 2018 |
| | Tanzania Bara | Endelea kupanua orodha ya kazi zenye hatari na shughuli zilizopigwa marufuku kwa watoto ili kuhakikisha kwamba orodha hiyo inajumuisha kupalilia na kusindika katika | 2016 – 2018 |

| Eneo | Chombo Husika | Hatua Iliyopendekezwa | Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa |
|---|---|---|---|
| | | uzalishaji wa tumbaku, karafuu, kahawa, katani na chai. | |
| | Zanzibar | Pitisha na chapisha sheria zinazoweka umri wa lazima kwa elimu. | 2018 |
| | Zanzibar | Hakikisha kwamba hakuna pengo kati ya umri wa elimu ya lazima na umri wa chini kabisa kwa kazi, linaloacha watoto wakumbwe kirahisi na ajira kwa watoto. | 2017 - 2018 |
| | | Hakikisha kwamba sheria haipigi marufuku upatikanaji wa elimu kwa wasichana wanaopata mimba na wavulana ambao hushiriki vitendo vya ngono. | 2017 - 2018 |
| | | Anzisha kisheria elimu bure ya msingi ya umma. | 2016 – 2018 |
| Utekelezaji | | Ongeza idadi ya wakaguzi wa kazi ili ulingane na ushauri wa kiufundi wa ILO. | 2013 – 2018 |
| | | Hakikisha kwamba afisa wa kazi thabiti ameteuliwa kwa kila mkoa, na chapisha taarifa hiyo. | 2013 – 2018 |
| | | Idhinisha wakaguzi wa kazi wa Tanzania Bara na Zanzibar kukadiria adhabu. | 2017 - 2018 |
| | | Chapisha taarifa za Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu hatua za utekelezaji wa sheria za ajira kwa watoto, kama vile ufadhili, mafunzo yaliyotolewa, ukaguzi wa kawaida na wa kushtukiza uliofanywa, ukiukwaji uliopatikana wa ajira kwa watoto, na adhabu zilizoamuriwa na malipo yaliyokusanywa. | 2011 – 2018 |
| | | Toa ufadhili wa kutosha na wafanyakazi wa kutosha waliofunzwa ili wafanye ukaguzi wa ajira kwa watoto. | 2013 – 2018 |
| | | Chapisha taarifa juu ya juhudi za utekelezaji wa sheria katika kupambana na ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na mafunzo yaliyotolewa, uchunguzi uliofanywa, ukiukwaji uliopatikana, mashtaka yaliyoanzishwa, na hukumu za hatia | 2012 – 2018 |

| Eneo | Chombo Husika | Hatua Iliyopendekezwa | Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa |
|---|---|---|---|
| | | za jinai zilizotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar. | |
| Uratibu | | Hakikisha kwamba Kikundi Kazi cha Elimu cha Kitaifa kuhusu Ajira kwa Watoto, Kamati ya Utendaji ya Zanzibar ya Ajira kwa Watoto, na Kamati ya Utendaji ya Ulinzi wa Kitaifa vinafanya kazi. | 2018 |
| Sera za Serikali | Tanzania Bara | Ondoa masharti katika Mtihani wa Kumaliza Shule ya Msingi na mitihani mingine ya kitaifa ambayo ni vizuizi kwa elimu, kama vile sera ya kutorudia mtihani tena. | 2016 - 2018 |
| | | Chukua hatua za kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Hatua za Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto nchini Tanzania. | 2018 |
| | Zanzibar | Hakikisha utekelezaji kamili wa sera ya Elimu ya Zanzibar ili kupunguza idadi ya wale wanaoacha masomo. | 2018 |
| Mipango ya Kijamii | | Shughulikia vizuizi kwa elimu, ikiwa ni pamoja na gharama za juu sana zinazohusika, kama vitabu, milo ya shuleni, na sare. | 2010 - 2018 |
| | | Unganisha mipango inayojumuisha ujenzi, huduma za majumbani, na sekta zisizo rasmi ili kushughulikia watoto wanaoshiriki katika ajira kwa watoto. | 2017 - 2018 |
| | | Chapisha habari kuhusu juhudi za serikali kupitia mipango ya kijamii inayoshughulikia ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na Kufanikisha Upunguzaji wa Ajira kwa Watoto ili Kuimarisha Elimu. | 2018 |